Je, Watanzania wanaionaje katiba?

Matokeo ya utafiti wenye uwakilishi wa kitaifa

1. Utangulizi

Tarehe 30 Desemba 2013, Tume ya Mabadiliko ya Katiba iliwasilisha rasimu ya pili ya katiba. Hii ilihitimisha kipindi cha kukusanya, kuchambua na kuyaweka pamoja maoni na mapendekezo ya wananchi na kuandaa rasimu iliyoboreshwa, pia kuashiria mwanzo Bunge la Katiba. Toleo la pili la rasimu ya katiba, pamoja na ripoti mbalimbali zilizoandaliwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba ni matokeo-kazi ya mwisho ya mchakato wa ushirikishwaji na kutafakari. Ni jinsi gani wananchi wanauona mchakato huu na wataiunga mkono rasimu ya pili ya katiba katika kura ya maoni?

Muhtasari huu unaripoti maoni ya hivi karibuni ya wananchi, kutoka Tanzania Bara na Zanzibar, juu ya rasimu ya katiba na maoni juu ya Bunge la Katiba. Matokeo muhimu kutoka Tanzania Bara yametokana na duru ya 14 ya *Sauti za Wananchi*, Utafiti wa kwanza Afrika kwa njia ya simu mkononi wenye uwakilishi wa kitaifa (www.twaweza.org/sauti).Takwimu zilikusanywa kutoka kwenye makundi ya wahojiwa Tanzania Bara. Simu zilipigwa kati ya tarehe 12 Februari 2014 na tarehe 4 Machi, 2014; takwimu hizi ni pamoja na majibu kutoka kaya 1547. Matokeo mengine yametokana na takwimu za duru ya tano ya utafiti wa *Sauti za Wananchi*, ambayo simu zilipigwa kati ya Julai 16 na Julai 30, 2013; takwimu hizi ni pamoja na majibu kutoka kaya 1,708 za Tanzania Bara. Kwa matokeo namba 4, 5 na 6, takwimu zilikusanywa kati ya tarehe 16 na 30 Julai 2013 Tanzania Bara tu.

Matokeo kutoka Zanzibar yanatoka duru ya sita ya *Wasemavyo Wazanzibari*, utafiti kwa njia ya simu ya mkononi wenye uwakilishi uliofanywa visiwani Zanzibar. Takwimu zilikusanywa kutoka kundi la wahojiwa maeneo yote ya Zanzibar. Simu zilipigwa kati ya Februari 24 na Machi 1, 2014; takwimu hizi ni majibu kutoka kaya 445.

Rasimu ya pili ya katiba ina vifungu 271 ambavyo vinaweka wigo mpana wa kupokea na kuvumilia fikra tofauti kwenye masuala yaliyopendekezwa. Kwa kutaka kupunguza idadi ya maswali, tuliweza kukusanya maoni juu ya sehemu ndogo ya masuala yaliyopendekezwa, ambayo yalichaguliwa kwa kuangalia masuala gani yalikuwa mada moto kwenye vyombo vya habari na yenye maslahi ya utawala kwa ujumla. Vipengele vingi muhimu, kama vile masuala yanayohusiana na umiliki wa ardhi, maliasili, elimu na huduma nyingine, uraia wa nchi mbili na haki za binadamu (*Bill of Rights*) havikufanyiwa kazi. Kwa hiyo, muhtasari huu unatoa maoni muhimu ya wananchi juu ya vifungu vidogo vya masuala yaliyopendekezwa, badala ya picha kamili ya vipaumbele vya wananchi

INTERNATIONAL LAW AND POLICY INSTITUTE
www.ilpi.org

Muhtasari huu umeandikwa na kuchapishwa na Twaweza, iliyopo Hivos Tanzania kwa kushirikishwa na ILPI.

S.L.P 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 22 266 4301-3 uwazi@twaweza.org
www.twaweza.org/sauti

Twaweza ni sisi

kuhusiana na rasimu ya katiba. Madhumuni yake ni kuchagiza midahalo makini na mijadala iliyojikita kwenye vipaumbele vya wananchi.

Matokeo muhimu kwenye muhtasari huu ni:[1]

- Robo ya Watanzania wanajua wapi wanaweza kupata nakala ya rasimu ya pili ya katiba na wananchi wengi wamefuatilia mijadala katika vyombo vya habari
- Idadi kubwa ya Watanzania wanaunga mkono vifungu vinavyohusiana na haki ya wananchi kupata taarifa au habari, na kuongezeka kwa uwajibikaji na uwazi wa viongozi wa umma
- Mapendekezo kwa ajili ya utaratibu wa kudhibiti na kuwajibisha wabunge na mgawanyo wa madaraka ili kuepuka migogoro ya kimaslahi yanaungwa mkono na wengi
- Maoni kuhusu muungano yamegawanyika pande zote mbili Tanzania Bara na Zanzibar
- Idadi kubwa ya Watanzania wanaunga mkono rasimu ya pili ya katiba

Matokeo haya yamefafanuliwa zaidi hapo chini. Katika hitimisho tunatafakari juu ya hatua za kusonga mbele, na tumetoa maoni yetu kuhusu uongozi unaotakiwa kutoka kwa wajumbe wa Bunge la Katiba na wengine ili kutunga katiba ambayo inawafaa wananchi wa Tanzania.

2. Mambo nane kuhusu rasimu ya pili ya katiba

Jambo la 1: Watanzania sita kati ya kumi wamesikiliza mjadala kuhusu rasimu mpya ya katiba

Tarehe 30 Desemba 2013, Tume ya Mabadiliko ya Katiba ilizindua rasimu ya pili ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kama ilivyokuwa kwa rasimu ya kwanza ya katiba zaidi ya mwananchi mmoja kati ya wanne (26%) kitaifa alijua mahali ambapo angeweza kupata nakala za rasimu ya katiba. Ukiangalia kwa undani zaidi, asilimia 87 ya Wazanzibari hawakujua wapi wangeweza kupata nakala ya rasimu ya pili ya katiba, ikilinganishwa na Tanzania Bara ambako asilimia 76 hawafahamu mahali pa kupata nakala ya rasimu ya katiba.

Kielelezo cha 1: Unajua wapi unaweza kupata nakala ya rasimu ya pili ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?



Chanzo cha Takwimu: *Sauti za Wananchi,* Utafiti - Awamu ya 14, Februari 2014 / *Wasemavyo Wazanzibari*, Utafiti – Awamu ya 6, Februari 2014

[1] Kwa ajili ya kusomeka mihutasari ya ripoti za Sauti za Wananchi hazijaweka wastani wa uwiano wa takwimu zilizotumika. Hata hivyo, zinapatikana kwa kuombwa na mtumiaji.

Kutokana na idadi hii, haishangazi kuona kuwa ni wananchi wachache ndiyo wameisoma rasimu ya pili ya katiba (takriban 3%, Kielelezo na 2). Hata hivyo, Watanzania sita kati ya kumi wamewahi kusikiliza mijadala kuhusu rasimu ya pili ya katiba kupitia luninga (TV), radio na mikutano ya wazi[2]. Wazanzibari wengi walieleza kuwa hawajawahi kuzungumzia/kufuatilia masuala ya rasimu ya katiba kwa njia yoyote.

Kielelezo cha 2: Ufuatiliaji wa wananchi rasimu ya pili ya katiba mpya



Chanzo cha Takwimu: *Sauti za Wananchi,* Utafiti - Awamu ya 14, Februari 2014 / *Wasemavyo Wazanzibari*, Utafiti - Awamu ya 6, Februari 2014

Jambo la 2: Wananchi wanawaamini wabunge kuwakilisha maslahi yao kwenye Bunge la Katiba

Bunge la Katiba limeundwa na wawakilishi kutoka makundi mbalimbali yanayojumuisha wabunge, vikundi vinavyotetea maslahi ya pamoja, wasomi na vyama vya wafanyakazi. Wananchi kutoka Tanzania Bara na Zanzibar wamebainisha kuwa wabunge ndiyo kundi bora litakalowakilisha vizuri zaidi maslahi yao kwenye Bunge la Katiba. Ni muhimu kufahamu kwamba Bunge la Katiba ndiyo lilikuwa limeanza wakati maswali haya yanaulizwa.

[2] Takwimu halisi kitaifa ni 61% na kwa Tanzania Bara ni 62%. Bara ina wastani mkubwa zaidi wa idadi ya watu ambao unajitokeza katika wastani wa takwimu zote za kitaifa.

Kielelezo cha 3: Nani atawakilisha vyema maslahi yako kwenye Bunge la Katiba?



Chanzo cha Takwimu: *Sauti za Wananchi,* Utafiti - Awamu ya 14, Februari 2014 / *Wasemavyo Wazanzibari*, Utafiti – Awamu ya 6, Februari 2014

Jambo la 3: Mapendekezo ya kuwepo kwa uwazi zaidi yanaungwa mkono na wengi

Tarehe 3 Juni 2013, Tume ya Mabadiliko ya Katiba ilizindua rasimu ya kwanza ya katiba na baadaye ilikusanya maoni na mwitikio wa wananchi. Kufuatia maoni na mwitikio wa wananchi pamoja na mashauriano zaidi Tume ya Katiba iliboresha rasimu ya katiba. Katika rasimu ya pili, idadi ya vifungu iliongezeka zaidi kutoka vifungu 240 hadi 271. Utafiti wa *Sauti za Wananchi* na *Wasemavyo Wazanzibari* ulichukua mapendekezo matano katika rasimu ya pili ambayo yanahusu uwazi na uwajibikaji hususan kuhusu watumishi wa umma. Mapendekezo haya yamekuwa na mvuto mdogo kwenye mijadala ya umma.

Hata hivyo, Kielelezo cha 4 kinaonesha mapendekezo haya yanaungwa mkono na wananchi wengi kutoka Tanzania Bara na Zanzibar. Watanzania kutoka Zanzibar wanaunga mkono kwa asilimia pungufu kidogo ya wenzao kutoka Tanzania Bara. Hata hivyo, kwa ujumla, kuna uungaji mkono mkubwa kwa mapendekezo ambayo yanalenga kuboresha upatikanaji huru wa taarifa vilevile uwazi kwenye umiliki wa mali binafsi kwa watumishi wa umma- iwe kwa mfumo wa zawadi, kuongeza utajiri au kumiliki akaunti za benki nje ya nchi.

Kielelezo cha 4: Maoni ya wananchi kuhusu uwazi na uwajibikaji
(Asilimia zilizooneshwa: "Nakubali"/"Nakubali kabisa")



Chanzo cha Takwimu: *Sauti za Wananchi*, Utafiti - Awamu ya 14, Februari 2014 / Wasemavyo Wazanzibari, Utafiti – Awamu ya 6, Februari 2014

Jambo la 4: Mapendekezo ya utaratibu wa kudhibiti na kuwawajibisha wabunge yanaungwa mkono na wengi

Pia kuna uungaji mkono mkubwa toka kwa wananchi (asilimia 70 au zaidi wanaafiki) uwepo wa viwango vya uwajibikaji na udhibiti wa wabunge. Kielelezo cha 5 kinaonesha kuwa wananchi wanaona wabunge wanapaswa kuwajibishwa kwa utendaji na majukumu yao kwa wapiga kura wao[3].

[3] Matokeo namba 4, 5 na 6 yametokana na utafiti duru ya mwezi Julai 2013 na yana majibu kutoka kwa wananchi wa Bara tu. Mapendekezo yaliyofanyiwa kazi yalikuwemo kwenye rasimu ya kwanza na yalibaki pia kwenye rasimu ya pili ya katiba

Kielelezo cha 5: Maoni ya wananchi kuhusu utaratibu wa kudhibiti na kuwajibisha wabunge



Chanzo cha Takwimu: *Sauti za Wananchi*, Utafiti - Awamu ya 5, Julai 2013

Jambo la 5: Mapendekezo kwa ajili ya ushindani zaidi kwenye uchaguzi yanaungwa mkono na wengi

Wananchi wengi wanaunga mkono hatua za kuimarisha ushindani wa kisiasa na kuwa na mamlaka huru inayosimamia uchaguzi. Kielelezo cha 6 kinaonesha wananchi asilimia 67 wanakubaliana na uwepo wa wagombea binafsi kugombea kiti cha Urais. Mara baada ya Rais kuchaguliwa, anapaswa kuteua chombo huru kusimamia uchaguzi, walisema Watanzania asilimia 65 waliohojiwa.

Kielelezo cha 6: Maoni ya wananchi kuhusu ushindani kwenye uchaguzi



Chanzo cha Takwimu: *Sauti za Wananchi*, Utafiti - Awamu ya 5, Julai 2013

Jambo la 6: Mgawanyo wa madaraka katika rasimu ya katiba unaungwa mkono na wengi

Kuna uungwaji mkono mkubwa wa mapendekezo katika rasimu ya katiba mpya yanayoboresha mgawanyo wa madaraka katika serikali. Kwanza, Spika au Naibu Spika lazima awe (aonekane kuwa) mtendaji huru, si kiongozi wa chama, wansema kwa mujibu wa maoni ya Watanzania asilimia 72. Pili, kuna wananchi wengi wanaunga mkono mapendekezo ya kutofautisha kwa uwazi kabisa majukumu ya kidemokrasia ya watendaji wakuu wa wizara (mawaziri au naibu mawaziri) kwa upande mmoja,

na wenye jukumu la kusimamia na kudhibiti watendaji (wabunge, madiwani) kwa upande mwingine. Watanzania saba kati ya kumi (70%) wanaunga mkono mgawanyo wa madaraka.

Kielelezo cha 7: Maoni ya wananchi juu ya mgawanyo wa madaraka



Chanzo cha Takwimu: *Sauti za Wananchi*, Utafiti - Awamu ya 5, Julai 2013

Jambo la 7: Maoni ya wananchi yamegawanyika kuhusu muundo wa serikali

Mapendekezo mawili zaidi yameshindwa kupata makubaliano ya wengi pande zote mbili Tanzania Bara na Zanzibar: mapendekezo hayo ni yale yaliyohusiana na muundo wa serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kielelezo cha 8 kinaonyesha kuwa Wazanzibari wengi (asilimia 80) wanaunga mkono muundo wa serikali tatu, wakati Tanzania Bara wanaounga mkono serikali tatu ni chini kidogo ya nusu (asilimia 43) ya wahojiwa.

Ni muhimu ieleweke kuwa miezi nane iliyopita wakati rasimu ya kwanza ilipopendekeza muundo wa serikali tatu, wananchi wa Tanzania Bara waligawanyika pia (asilimia 51 waliunga mkono serikali tatu). Kwa upande mwingine, ni wananchi wa Tanzania Bara ndiyo wanaotaka maliasili zote zisimamiwe kwenye ngazi ya serikali za kila upande (Tanzania Bara/Zanzibar)-siyo ngazi ya serikali ya muungano.

Kielelezo cha 8: Maoni ya wananchi kuhusu muundo wa muungano (asilimia iliyooneshwa: "Nakubali"/"Nakubali kabisa")



Chanzo cha Takwimu: Sauti za Wananchi, Utafiti - Awamu ya 14, Februari 2014 /

Wasemavyo Wazanzibari, Utafiti – Awamu ya 6, Februari 2014

Kutokana na ukweli kuwa mijadala mingi baada ya uzinduzi wa rasimu ya kwanza na ya pili ya katiba ilijikita kwenye muundo wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Watanzania waliulizwa kubainisha mabadiliko gani (kama yapo) wangependa kuyaona kwenye muungano kati ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Kielelezo cha 9 hapo chini kinaonesha kuwa Wazanzibari aidha wanataka uhuru zaidi kujitawala au muungano wa serikali tatu. Wananchi kutoka Tanzania Bara wamegawanyika nusu kwa nusu juu ya muundo wa serikali wanaoutaka. Miezi nane iliyopita Watanzania kutoka Bara walikuwa wazi zaidi wakiunga mkono uhuru zaidi wa Zanzibar kujitawala (asilimia 32).

Kielelezo cha 9: Mabadiliko gani (kama yapo) ungependa kuyaona kwenye muungano kati ya Tanzania Bara na Zanzibar?



Chanzo cha Takwimu: Sauti za Wananchi, Utafiti - Awamu ya 14, Februari 2014 / Wasemavyo Wazanzibari, Utafiti – Awamu ya 6, Februari 2014

Jambo la 8: Rasimu ya sasa ya katiba ina uungwaji mkono wa kutosha kupitishwa

Baada ya Bunge la Katiba kupitia na kurekebisha rasimu ya pili ya Katiba itaandaliwa rasimu ya tatu na ya mwisho. Ili rasimu ya mwisho ipitishwe na kuwa sheria kamili itahitaji kupigiwa kura ya maoni na wananchi ambapo ni lazima ipitishwe kwa nusu ya kura zote (asilimia 50 ya kura zote +1) pande zote mbili Tanzania Bara na Zanzibar.

Kama wananchi wangeipigia kura ya maoni Rasimu ya Katiba, kwa maoni yao ya sasa (Februari 2014), katiba ingepitishwa- hata kama wale ambao hawajaamua wangepiga kura kuipinga. Kama ilivyooneshwa katika Kielelezo cha 10, zaidi ya asilimia 60 ya wapiga kura kutoka Tanzania Bara na Zanzibar walisema wana nia ya kupiga kura ya kuikubali katiba kama ilivyo sasa.

Kielelezo cha 10: Je, ungepiga kura kuikubali au kuipinga rasimu ya pili ya katiba?



Chanzo cha Takwimu: Sauti za Wananchi, Utafiti - Awamu ya 14, Februari 2014 / Wasemavyo Wazanzibari, Utafiti – Awamu 6, Februari 2014

3. Hitimisho

Tangu mapema mwezi Februari mwaka 2014, wakati kiasi kikubwa cha takwimu katika muhtasari huu zilipokusanywa, Watanzania wengi wamefuatilia mjadala katika Bunge la Katiba kuhusu rasimu ya pili ya katiba. Wakati mjadala umevuta hisia za wengi na kutangazwa kwa upana na vyombo vya habari, mwelekeo wa mjadala mara nyingi umeonekana kuwagawa wajumbe pande mbili na kuchukiza umma, huku ukiibua maswali kuhusu viwango vya Bunge la Katiba kuhudumia na kutetea maslahi ya umma. Hakika suala la kuhoji kama maoni yaliyokusanywa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba yawakilisha matakwa ya umma limekuwa suala la mabishano. Maoni ya wananchi ni muhimu pia kwa sababu, bila kujali nini kinaamliwa na wawakilishi kwenye Bunge la Katiba, watu watakuwa na uamuzi wa mwisho wakati rasimu ya katiba inapigiwa kura ya maoni.

Hivyo basi, wananchi wa kawaida wanafikiri na kupendelea nini hasa? Nguvu ya muhtasari huu ni kwamba unatoa takwimu za kuaminika juu ya mapendekezo ya wananchi kutoka pande zote za Muungano, kwa kutumia mbinu ambazo ni huru na makini kisayansi. Takwimu hizi zinatoa fursa kwa wajumbe wa Bunge la Katiba na wananchi kwa ujumla kutafakari kwa makini juu ya jambo hili na kujenga upya muafaka wa kitaifa.

Idadi kubwa ya wananchi wanataka kuwa na katiba inayoakisi muafaka mpya kati ya dola na wananchi. Masuala yanayohusiana na matumizi ya madaraka, kupata habari na udhibiti wa viongozi na watumishi wa umma yanaungwa mkono na wananchi wengi nchini kote. Masuala haya ni pamoja na "mtumishi wa umma kutoshiriki kufanya maamuzi juu ya kitu au shughuli yoyote ambayo ni ya manufaa binafsi," "watumishi wa umma wanatakiwa kutangaza na kuwasilisha orodha ya mali zao na madeni" na "watumishi wa umma kutoruhusiwa kumiliki akaunti ya benki nje ya nchi." Mapendekezo mengine kama hayo ni pamoja na kuweka ukomo kwa wabunge kugombea kwa vipindi vitatu na haki ya wananchi kumwondoa mbunge wao iwapo ameshindwa kuwajibika kwa wapiga kura wake.

Pia kuna uungwaji mkono mkubwa kutoka kwa wananchi wanaotaka kuona uwanja wa siasa, kanuni huru za vyama vya siasa na sheria zinazotoa fursa za kugombea zinatoa haki zaidi kwa wananchi, kama vile haki ya wagombea binafsi kugombea kwenye uchaguzi, kuanzisha chombo cha kusimamia uchaguzi ambacho ni huru kabisa, wabunge kutoteuliwa kuwa mawaziri katika serikali, na Spika na

Naibu Spika wa Bunge kutokuwa wanachama wa chama chochote cha siasa. Haya yanaonesha kuwa wananchi wanataka kuwe na utaratibu kina zaidi wa dola kudhibitiana, na kuwa na taasisi za serikali kama vile tume ya uchaguzi na bunge vikifanyakazi kikamilifu kusimamia na kudhibiti serikali.

Ukweli kwamba mchakato wa Bunge la Katiba hadi sasa umetawaliwa na hoja kuhusu utaratibu wa kanuni na muundo wa Muungano, badala ya masuala haya yanayowagusa zaidi wananchi, ni jambo la kusikitisha. Bunge la Katiba na viongozi wa serikali na vyama vya siasa, wakitaka kuvitendea haki vipaumbele vya watu, watafanya vyema kuyapa umakini wa kutosha masuala haya yanayohusiana na uwajibikaji kwa umma.

Pamoja na haya, matokeo ya utafiti katika muhtasari huu yanathibitisha kuwa wananchi wamegawanyika juu ya muundo wa Muungano. Tanzania Bara asilimia 43 wanaunga mkono pendekezo la uwepo wa serikali tatu; wakati Zanzibar asilimia 80 wanaunga mkono serikali tatu. Aidha, asilimia 53 ya Wazanzibari inaonesha kuwa kuikubali rasimu ya pili ya katiba itategemea pendekezo hili. Iwapo rasimu ya mwisho ya katiba itarejea kwenye serikali mbili, na kwa kuzingatia yaliyosemwa na wananchi sasa (Februari 2014) haiko wazi kama wananchi wengi kutoka pande zote za Muungano wataunga mkono katiba mpya.

Njia moja ya kutoka kwenye mkwamo huu ni kutumia taswira ya masuala ya msingi ya utawala ambayo ni vipaumbele vya wananchi pande zote mbili za Muungano - kama vile nani ana haki ya kujua nini, umiliki wa rasilimali za umma, na uwajibikaji wa watumishi wa umma – kuelewa muundo wa muungano una maana gani zaidi, kuliko kujikita kwenye misimamo ya vyama. Kwa namna nyingine, tunaweza kujiuliza muundo wa serikali mbili au tatu una maanana athari gani kwenye masuala kama vile haki na usalama wa kumiliki mali, uhuru wa kujieleza, haki ya kupata huduma za msingi, mshikamano wa kijamii na haki za wachache?

Jinsi ya kutatua hali hii si jambo rahisi, lakini huo ndiyo wajibu unaotakiwa wa uongozi. Uongozi wa kweli siyo kutetea kwa nguvu msimamo na maslahi yako mwenyewe, lakini kudadisi mitazamo na maoni mbalimbali, na kujenga makubaliano mapya kulingana na kanuni za msingi na maslahi ya pamoja.